JARIDA LA

# UMASKINI NA MAZINGIRA

ISSN 0821-6528

Hutolewa Mara Mbili kwa Mwaka na Ofisi ya Makamu wa Rais

Toleo la 6


JAN. - JUNE 2009

# Ziara ya Katibu Mkuu Mbarali yatoa sura mpya kwa sekta ya mazingira



HUTOLEWA MARA MBILI KWA MWAKA NA OFISI YA MAKAMU WA RAIS

JARIDA LA
UMASKINI
NA MAZINGIRA




**Picha ya Jalada:** Mandhari ya safu za milima ya Livingstone

# Lengo la Jarida la Umaskini na Mazingira

Jarida hili linatolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR), Idara ya Mazingira kwa ufadhili wa Mradi wa Umaskini na Mazingira kwa lengo la kutoa elimu na kujenga uelewa wa jamii na wadau mbalimbali kuhusu uhusiano uliopo kati ya umaskini na mazingira. Taarifa na makala zilizochapishwa katika jarida hili, zitatoa elimu na maarifa kwa watu binafsi na jamii kwa ujumla, na hatimaye kuchangia katika usimamizi endelevu wa mazingira katika utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA)

## Yaliyomo:


- Juhudi za Kuondoa Umaskini kwa wakazi wa Jiji la Dar zitabaki kuwa Ndoto Kama Uchafuzi wa Mazingira hautadhibitiwa!!!........................................................ 3
- Katibu Mkuu Atembelea Mbeya na Kupongeza Jitihada za Utunzaji wa Mazingira ......................................... 4
- Kupunguza Gesijoto Kupitia Kudhibiti Ukataji Miti Na Uharibifu Wa Misitu Katika Nchi Zinazoendelea...... 7
- Utunzaji wa Mazingira Wasaidia Vijana Kujitegemea... 9
- Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Hifadhi ya Mazingira katika Uchimbaji Madini kuchangia Juhudi za uchimbaji endelevu Tanzania............................. 12



**Bodi ya Uhariri**

**Mwenyekiti**
Eric Mugurusi

**Wajumbe**
Bonaventura Baya
Angelina Madete
Anna Maembe
Blandina Cheche

**Mshauri**
Siglinda Chipungaupi

**Usanifu na Uchapaji**
Penplus Ltd.

# Juhudi za Kuondoa Umaskini kwa wakazi wa Jiji la Dar zitabaki kuwa Ndoto Kama Uchafuzi wa Mazingira hautadhibitiwa!!!

**Na Glory Kombe na Anna Maembe**

Tarehe 11 – 15 Machi mwaka huu (2009), Mheshimiwa Waziri Mkuu – Mizengo Pinda alifanya ziara katika baadhi ya maeneo ya manispaa zote tatu za jiji la Dar es Salaam ili kuangalia hali ya mazingira kwa ujumla na shughuli za maendeleo za wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira kutoka NEMC, Dk Robert Ntakamulenga alikuwa mmoja wa watalamu walioongozana na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea maeneo kadhaa; baadhi ya maeneo haya ni pamoja na masoko ambako wakazi wa jiji hujipatia mahitaji yao. Masoko haya ni Kigogo, Buguruni, Michikichini, Kariakoo, Tandale, na Soko la samaki la Feri.

Aidha Waziri Mkuu alitembelea kituo cha Mabasi yaendayo mikoani cha Ubungo, Kiwanda cha Nguo cha Karibu kilichoko Mbagala, Dampo la Kisasa lililoko Pugu Kinyamwezi, mabwawa ya majitaka yaliyoko Buguruni na dampo la Kigogo,

Ziara hii ilibainisha kuwa maeneo mengi ya jiji ni machafu na hali yake hairidhishi kimazingira na ni hatari kiafya. Baadhi ya mambo yanayosababisha hali hiyo ni:-

i) Utupaji holela wa taka (littering) unasababisha mlundikano wa taka hasa katika masoko na mitaa ya jiji unaochangia kusababisha magonjwa kama malaria na yale ya mlipuko kama kipindipindu na homa ya matumbo.

ii) Kuziba kwa mitaro ya maji ya mvua hivyo kufanya maji kutuama kwa muda mrefu hasa wakati wa msimu wa mvua, hivyo kusababisha mazalia ya mbu wanaosababisha malaria.

iii) Nyumba nyingi zimechakaa kwa kukaa muda mrefu bila kupakwa rangi hivyo kufanya majengo mengi kuonekana kama magofu.

iv) Utiririshaji ovyo wa majitaka taka majumbani na viwandani kuingia kwenye mazingira hasa maeneo ya Mto Kizinga huko Mbagala na Mlalakuwa.

v) Uchafuzi unaotokana na gesi taka na moshi hasa kutoka viwandani na vyombo vya usafiri kama magari.

vi) Biashara kufanyika katika njia za watembea kwa miguu na maeneo yasiyoruhusiwa hivyo kuchangia kuchafua na kuharibu mandhari ya jiji.

Mwisho wa ziara yake, Waziri Mkuu alitoa maagizo kwa manispaa zote na watendaji wa Mkoa wa DSM kuchukua hatua za haraka kushughulikia kero za jiji hasa ukusanyaji na uzoaji taka pamoja na kuhakikisha dampo la Kigogo lililoko katika makazi ya watu vinashughulikiwa mara moja. Pia aliagiza mkataba unaohusu ukusanyaji wa mapato katika kituo cha mabasi yaendayo mikoani cha Ubungo uangaliwe upya. Aidha taarifa kuhusu hatua zilizochukuliwa kushughulikia kero za wananchi kama masuala ya uzoaji taka, kuziba kwa mitaro ya maji machafu na ya mvua ipelekwe katika ofisi yake ambayo ndiyo wizara mama ya halmashauri zote nchini.

Baada ya ziara ya Waziri Mkuu, NEMC kwa kushirikiana na manispaa tatu za jiji la DSM ilifanya ukaguzi wa kina wa mazingira katika manispaa zote kwa kutumia wakaguzi wake walioteuliwa hivi karibuni. Ukaguzi huu ulishirikisha manispaa husika, hususan, Maafisa Mazingira wa manispaa, Watendaji wa Kata na Wenyekiti wa Mitaa. Ukaguzi pia ulilenga kuwaelekeza maafisa mazingira wa manispaa na watendaji wa mitaa jinsi ya kukagua na kuchukua hatua kwa kutumia Sheria ya Mazingira Sura 191 ya mwaka 2004. Ziara hii ililenga pia kuwasaidia maafisa mazingira kubaini vyanzo vya uchafuzi wa mazingira na kushauri uongozi wa manispaa

>>> inaendelea uk. 8

# Katibu Mkuu Atembelea Mbeya na Kupongeza Jitihada za Utunzaji wa Mazingira

**Na Dkt Constantine M. Shayo**

Katibu Mkuu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Bibi Ruth H. Mollel alifanya ziara ya kikazi mkoani Mbeya kuanzia tarehe 1 Mei 2009 hadi 4 Mei 2009 ili kujionea utekelezaji wa shughuli mbalimbali za utunzaji wa mazingira katika Mkoa huo. Katika ziara hiyo, Bibi Mollel aliambatana na wataalamu wa mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.



*Kambi ya askari wa wanyamapori waliohusika katika zoezi la kuhamisha mifugo kutoka Ihefu*

Ziara hiyo ilianzia katika wilaya ya Mbarali ambako Katibu Mkuu na ujumbe wake walikutana na uongozi wa Wilaya ambao uliwasilisha taarifa ya wilaya kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za usimamizi wa mazingira wilayani hapo.

Wilaya ya Mabarali ni wilaya muhimu katika uzalishaji wa mazao ya chakula kama mpunga, mahindi na alizeti. Kuna miradi ya umwagiliaji ambayo ni tegemeo kubwa la nchi kwa uzalishaji wa mpunga. Aidha, bonde la Ihefu ni chanzo cha maji yanayoingia katika Mto Ruaha Mkuu na Bwawa la Mtera ambalo ni mojawapo ya chanzo muhimu cha uzalishaji wa umeme nchini.

Kutokana na tatizo la wingi wa mifugo na uhaba wa malisho na maji hususan katika mikoa ya Mwanza, shinyanga na Arusha, wafugaji walilazimika kuhama na mifugo yao na kuvamia bonde oevu la Ihefu. Inakadiriwa kuwa mwaka 2005 kulikuwa na idadi ya ng'ombe 350,000, mbuzi 140,000 na kondoo 100,000 katika bonde oevu la Ihefu. Matokeo ya uvamizi huu ni kwamba, maji yalipungua sana katika bonde hili na kusababisha uoto wa asili, wanyama pori, ndege wanaohamahama na bioanuai zingine kupotea. Hali hii ilisababisha kina cha maji katika bwawa la Mtera kupungua kiasi kikubwa hususan mwaka 2005, ambapo uzalishaji wa umeme ulipungua kwa kiasi cha kusababisha mgao wa umeme nchini na kuathiri shughuli za kiuchumi.

Mwaka 2006, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau na sekta nyingine iliandaa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji Nchini. Mkakati huu ulianisha changamoto 12 ambazo zilitakiwa kushughulikiwa haraka na moja ya changomoto hizo ilikuwa ni kuondoa mifugo iliyovamia vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na bonde la Ihefu. Mwaka 2006 mifugo yote iliyokuwa imevamia bonde la Ihefu ilihamishwa. Aidha Serikali iliamua kulitangaza bonde la Ihefu kama sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ili kuokoa chanzo hiki cha maji na kuzuia uvamizi wa wafugaji kutokea tena.



*Baadhi ya ng'ombe waliokuwa katika ardhi oevu ya Ihefu*



*Katibu Mkuu akipewa maelezo kuhusu hali ya mazingira ya bonde la Ihefu*

Baada ya kupata maelezo kutoka kwa uongozi wa Wilaya, Katibu Mkuu na ujumbe wake walipata fursa ya kutembelea bonde la Ihefu na kujionea jinsi uoto wa asili ulivyorudia hali yake ya awali baada ya mifugo kuhamishwa na kina cha maji katika bonde kuongezeka ukilinganisha na hali ilivyokuwa kabla ya mifugo kuondolewa. Aidha wajumbe walijionea wanyama na ndege wa aina mbalimbali walioanza kurudi.

Bonde la Ihefu ni kivutio kikubwa cha utalii hususan utalii wa *"Yatch"* na uvuvi wa kitalii. Katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na wavamizi, TANAPA imeimarisha ulinzi dhidi ya wavamizi kwa kuongeza idadi ya walinzi na vifaa vya doria.




*Ramani inayoonyesha sehemu ilipo Hifadhi ya Taifa ya Kitulo*

Japokuwa mafanikio yameonekana katika kulihifadhi eneo hili na kutunza mazingira, kwa ujumla bado nguvu kubwa inahitajika ili kuwaelimisha baadhi ya wakazi ambao hawajahama katika eneo hili ili kupisha Hifadhi. Kwa mujibu wa taarifa ya uongozi wa wilaya, tayari kesi mbili zimefunguliwa, moja katika Mahakama Kuu kanda ya Kusini dhidi ya Uongozi wa wilaya ya Mbarali na nyingine katika Mahakama ya Kuu ya Ardhi dhidi ya TANAPA zikipinga kuondolewa kwa wananchi hao katika eneo hili ambalo ni rasilimali kubwa kwa uchumi wa Tanzania.


Taarifa ya Wilaya ilieleza kuwepo na malalamiko kuwa wawekezaji na watumiaji wengine wa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji wamekuwa wakihodhi maji bila kuyarudisha kwenye mkondo wake. Hali hii inaweza kuathiri juhudi za kuhifadhi eneo hili na mustakabali wa mazingira katika maeneo haya.

Aidha rai imetolewa kwa TANAPA kuangalia uwezekano wa kuruhusu wananchi kujipatia kipato kwa kufanya shughuli nyingine kama ufugaji wa nyuki katika maeneo yaliyohifadhiwa ili kujikomboa kiuchumi. Bibi Mollel alishauri Mkoa uchukue jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa maji yanayotumika katika umwagiliaji yanarudishwa kwenye mkondo wake baada ya matumizi na wawekezaji au wakulima wasiruhusiwe kuchukua maji mengi kuliko mahitaji. Aidha alishauri Hifadhi ya Ruaha ianze kutangaza fursa za utalii katika bonde la Ihefu kama utalii wa kutumia boti (yatching/ canoeing) na uvuvi (spot fishing).

Aidha, Bibi Mollel alitembelea Hifadhi ya Taifa ya Kitulo yenye ukubwa wa kilomita za mraba 465.4 inayojumuisha eneo lillilokuwa shamba la mifugo la Kitulo na misitu miwili ya serikali ya Livingstone na Numbe.

Mwaka 1965-1968 eneo hili lilikuwa chini ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa ajili ya majaribio ya kilimo kwa uzalishaji wa nafaka (ngano) na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, nyama pia na kondoo wa sufi. Mwaka 1968-1975 Kitulo ilikuwa chini ya kampuni iliyoitwa "National Agricultural Ranching Company" (NARCO) wakiendeleza shughuli za uzalishaji wa ngano, maziwa, nyama na sufi.

**>>> inaendelea uk. 6**



*Sehemu ya Jengo la Machinjio ya Ipinda*

# Katibu Mkuu Atembelea Mbeya...

>>> inatoka uk. 5

Kwa kutambua umuhimu wa eneo la Kitulo, mwaka 2002 Serikali iliikabidhi Wizara ya Maliasili na Utalii kulisimamia na ikateua TANAPA kuliendesha. Mchakato mzima wa uanzishwaji wa Hifadhi ulikamilika 16/9/2005. Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ilitangazwa tarehe 16 Septemba 2005.

Katibu Mkuu alifika Kitulo eneo lenye vyanzo vikuu vya maji vinavyounda mito mikubwa inayomwaga maji katika Ziwa Nyasa na Mto Ruaha Mkuu. Aidha,aliweza kukagua mazingira ya eneo hili ambalo hupatikana mimea, ndege na wanyama adimu wasiopatikana kwingineko nchini na duniani kwa ujumla. Pia ni makazi ya muda ya ndege wahamao katika mabara ya Afrika na Ulaya. Eneo hili ni la uwanda mpana wa nyasi wenye mandhari nzuri.

Shughuli za hifadhi ya mazingira zimesaidia kuimarisha uoto wa asili na vyanzo muhimu vya maji vimeboreka kwa kiasi kikubwa. Uongozi wa Hifadhi imegharamia miradi ya maendeleo ya wananchi (kama shule, zahanati, na ujasiriamali) katika Wilaya za Makete na Rungwe. Idadi ya watalii imeanza kuongezeka ambapo mwaka 2007/08, idadi ya watalii walikuwa takriban 150 na katika kipindi cha nusu ya kwanza ya 2008/09, idadi ya watalii ilifikia 180. Ni dhahiri kuwa shughuli hizi za kiuchumi zitasaidia kupunguza umaskini kwa ujumla.



*Katibu Mkuu OMR akisalimiana na wanafunzi wa Shule ya sekondari, Matema Beach*

Ujumbe wa Katibu Mkuu pia ulitembelea Wilaya ya Kyela na kukutana na Uongozi wa Wilaya (DED, na Wakuu wa Idara) ambapo Taarifa ya Wilaya na Mpango wa Mazingira wa Wilaya ilitolewa. Baada ya taarifa hiyo, ujumbe pamoja na baadhi ya wenyeji ulitembelea na kukagua mazingira ya Machinjio katika eneo la Ipinda,



*Mandhari ya safu za milima ya Livingstone*

Shule ya Sekondari ya Matema Beach, safu za milima ya Livingstone na fukwe za Ziwa Nyasa katika eneo la Lyulilo - Matema Beach.

Takwimu zinaonesha kuwa wilaya ya Kyela ni miongoni mwa wilaya ambazo zimevuka lengo la kupanda miti zaidi ya milioni moja na nusu kwa mwaka kama ilivyoelekezwa katika Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Taasisi mbalimbali zimechangia kufikia lengo hili zikiwamo shule na hoteli, kwa mfano Hoteli ya Matema Beach inayozingatia usafi wa Mazingira, na kupanda na kutunza miti. Mazao mengi yanayozalishwa wilayani Kyela yanatokana na miti, hivyo kuifanya wilaya ifunikwe na aina mbali mbali za miti ya matunda kama miembe, korosho na kakao.

Aidha, Bibi Mollel aliweza kuona changamoto zilizojitokeza, kwa mfano katika kijiji cha Lyulilo ambako kilimo katika miteremko mikali kimesababisha mmomonyoko wa udongo katika sehemu za safu za milima ya Livingstone, eneo la Matema Beach.

Kwa ujumla Mkoa wa Mbeya umefanya vizuri katika kuhifadhi vyanzo vya maji, kupanda na kutunza miti. Bibi Mollel alishauri jitihada hizi ziendelee na wananchi waliovamia miteremko ya milima na wale wanaofanya uchafuzi wa fukwe za Ziwa Nyasa wahamishwe. Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji unaeleza kuwa maeneo ya namna hii hayaruhusiwi kufanyika kwa shughuli zozote za binadamu.

# Kupunguza Gesijoto Kupitia Kudhibiti Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu Katika Nchi Zinazoendelea: Mpango Unaolenga Kusaidia Usimamizi Endelevu wa Misitu na Kupunguza Umasikini Nchini

**Patrick M. Ndaki**

Dhana ya kupunguza gesijoto kupitia kudhibiti ukataji miti na uharibifu wa misitu katika nchi zinazoendelea inatokana na uelewa wa jumuiya ya kimataifa kuwa tatizo la mabadiliko ya tabianchi linaendelea kuwa tishio kwa mazingira ya asili, afya ya binadamu, uwezo wa kujipatia mahitaji pamoja na maendeleo ya kiuchumi, hasa kwa nchi masikini kama Tanzania. Inafahamika kwamba mifumo ikolojia ya misitu hutumika kunyonya na kutunza hewa mkaa. Ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu katika nchi zinazoendelea kama Tanzania ni mojawapo ya sababu zinazoripitiwa kuchangia uzalishaji wa hewa mkaa. Jopo la Umoja wa Mataifa la wataalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi linakadiria kuwa ukataji miti na uharibifu wa misitu unachangia kwa asilimia kati ya 18-20 uzalishaji wa gesijoto duniani.



*Ukataji wa misitu unasababisha ongezeko la gesijoto.*

Tanzania inakadiriwa kuwa na jumla ya hekta milioni 35.3 za eneo la misitu. Kati ya hekta hizo, hekta milioni 16 ni hifadhi za misitu, hekta milioni 2 ni misitu katika Hifadhi za Taifa hekta milioni 17.3 zilizobaki, ikiwa ni asilimia 49, ni maeneo mengine yenye misitu ambayo hayako katika hifadhi ambayo yako katika hatari kubwa ya kuharibiwa kupitia kilimo cha kuhamahama, uchomaji moto, ukataji wa misitu kwa ajili ya kuni na mkaa, ujenzi, mbao pamoja na maeneo ya misitu kubadilishwa matumizi, mfano kilimo, ufugaji, makazi na maendeleo ya viwanda. Kiwango cha ukataji miti na uharibifu wa misitu kinakadiriwa kuwa hekta 412,000 kwa mwaka.

Njia mbalimbali za usimamizi na uhifadhi wa misitu katika ngazi za kitaifa na kimataifa huchangia katika juhudi za kupunguza gesijoto na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Usimamizi endelevu wa misitu unachangia katika juhudi za kupunguza gesijoto na kuendeleza uhifadhi wa hewa mkaa na hivyo kusaidia katika kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi

Biashara ya hewa mkaa kwa sasa inapata umaarufu na kuna soko linalo kua kwa ajili ya kupunguza hewa mkaa kupitia misitu duniani. Ni kutokana na hali hiyo, suala la kupunguza uzalishaji wa hewa mkaa kupitia kudhibiti ukataji miti na uharibifu wa misitu sasa ni sera mpya ya mabadiliko ya tabianchi duniani ikihusisha nchi zilizoridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi inayolenga kutoa fedha kwa ajili ya nchi na jamii zinazojihusisha katika juhudi za kupunguza ukataji miti na uharibifu wa misitu katika nchi zinazoendelea. Majadiliano kuhusu suala hili yalianza mwaka 2005 mjini Montreal. Hatua kubwa ilifikiwa katika mkutano wa 13 wa nchi zilizoridhia Mkataba kwa kupitisha uamuzi unaozitaka nchi wanachama kuandaa ziandae mikakati na kutekeleza miradi ya majaribio ya kupunguza gesijoto kwa kudhibiti ukataji miti na uharibifu wa misitu.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotekeleza shughuli za kupunguza hewa mkaa kupitia udhibiti wa ukataji miti na uharibifu wa misitu katika kipindi cha majaribio. Utekelezaji wa shughuli hizi unalenga: kuunga mkono

>>> inaendelea uk. 10

## Juhudi za Kuondoa Umaskini kwa wakazi wa Jiji la Dar...

>>> inatoka uk. 3

kuchukua hatua zinazostahili kurekebisha hali hiyo kwa kutumia sheria za halmashauri au sheria ya mazingira.

Katika Manispaa ya Temeke, kata za Keko, Chang'ombe na Kurasini zilikaguliwa. Wakaguzi walibaini kutokuwepo mfumo wa ukusanyaji wa taka ngumu, ujenzi holela wa makazi , ukosefu wa miundombinu ya majitaka yatokayo majumbani na ya mvua. Aidha baadhi ya maeneo katika kata hizi hayana maji safi na salama (hakuna mabomba), changamoto ambazo kama hazikutafutiwa ufumbuzi mapema zitaendelea kuwaongezea wananchi umaskini kutokana na maradhi kama malaria, kipindu pindu na kuharisha yanayowapata wakazi hawa mara kwa mara. Maradhi haya huwafanya wakazi kutumia pesa nyingi kujitibu na kupoteza muda mwingi ambao ungetumika kwa shughuli mbali mbali za maendeleo.

Ukaguzi pia ulibaini kuwa kukosekana kwa mfumo wa kuondosha taka ngumu katika makazi kunatokana na wakazi kushindwa kulipia gharama za wakandarasi wa kuzoa taka katika maeneo hayo. Aidha, nyumba nyingi zimejengwa katika maeneo yasiyopimwa na nyingine ziko katika maeneo hatarishi kama maeneo oevu (wetlands). Kukosekana miundombinu ya kuondosha majitaka ya majumbani na ya mvua na wakazi wengi kutumia vyoo vya shimo katika maeneo kama haya ambayo kina cha maji (water table) kiko juu. Vyoo hivyo hufurika hasa wakati wa mvua na uchafu huo kuingia katika makazi ya watu na mazingira na kusababisha kero na madhara kiafya. Aidha hali hii husababisha maradhi yanayochukua muda mwingi wa kuzalisha mali na pia pesa kwa ajili ya matibabu.

Aidha maji safi na salama kwa wakazi hayapatikani kwa urahisi kutokana na kutokuwa na mfumo wa maji ya bomba, hali inayobabisha wakazi kuchimba visima vifupi katika makazi yao. Kulingana na hali ya mazingira katika maeneo haya, maji haya yanakuwa yamechafuliwa na yana vimelea vya magonjwa mbalimbali hasa ya tumbo kama kipindupindu, kuhara na homa ya matumbo.

Taka ngumu zinazozalishwa majumbani na zinazotokana na biashara ndogo ndogo zinatupwa ovyo katika mifereji ya maji ya mvua. Hali hii inasababisha mifereji kuziba na kusababisha maji machafu kutuama kwa muda mrefu na kuwa mazalia ya wadudu hatari kama mbu waenezao malaria.

Kwa kiwango kikubwa taka na uchafu unachangia uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya makazi. Kutokana na uchafuzi wa mazingira, magonjwa mbalimbali yanawapata wakazi hivyo kupoteza muda na pesa kwa matibabu na muda mwingi ambao ungetumika katika shughuli za maendeleo na za kijamii na taifa kwa ujumla.

Akiongea na mmoja wa wandishi wa makala hii, Bwana Sixtus Chaduma, mkazi wa Tandale kwa Mtogole jijini DSM ambaye ni kibarua wa mafundi ujenzi, alisema kuwa kwa mwezi wa Februari (2009) pekee, yeye, mkewe pamoja na mwanae wametumia kiasi cha shilingi 28,000 kununua dawa za malaria (Alu na panadol dozi tatu) na za tumbo (Amoxcylin). Kiasi hiki cha pesa kingeokolewa na kufanya shughuli za maendeleo endapo taka na uchafu vingezolewa. Bw. Chaduma aliongea huku akionyesha vyeti vyake na risiti alizonunulia dawa.

Kama huyu mkazi mmoja tu anatumia shilingi 28,000 kwa mwezi na kama ataumwa malaria kila mwezi mara moja kwa mwaka mzima, gharama ya matibabu pekee ni shs 336,000/. Bw Chaduma alieleza kuwa hupata kati ya shs 6000 mpaka 10,000 kwa siku kwa siku 6 kwa wiki, kiasi ambacho ni wastani wa shs 2,496,000 kwa mwaka. Kwa kutumia shs. 336,000 kwa matibabu basi asilimia 13.5 ya kipato chake cha mwaka mzima hutumika kwa matibabu. Je akiokoa kiasi hiki kwa kufanya usafi si zitamsaidia katika shughuli za maendeleo kama kulipia ada ya mwanae au kuanzisha mradi mdogo wa kumwongezea kipato? Ni bora kuzuia kuliko kutibu na gharama ya kufanya usafi ni ndogo sana ukilinganisha na kugharamia matibabu.

Pamoja na maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu kwa Halmashauri ya jiji pamoja na Manispaa zake, Baraza linaongezea kushauri halmashauri husika kuweka mipango madhubuti ya kuboresha makazi haya (upgrading) kwa kuweka miundo mbinu ya uondoshaji taka, kwa ajili ya maji safi na salama na kufanya ukaguzi wa usafi mara kwa mara ili kubaini wakazi wasioweka mazingira yao safi na kuwachukulia hatua kwa kutumia

>>> inaendelea uk. 9

# Utunzaji wa Mazingira Wasaidia Vijana Kujitegemea

### Waacha kupiga debe na kuwa wakulima

**Na G. Aliti**

Mji wa Kibondo upo kilomita 244 Kusini mashariki ya Makao makuu ya Mkoa wa Kigoma na ni mojawapo ya wilaya tano za mkoa wa Kigoma. Kwa mtu anayesafiri kuelekea Kibondo, atafurahia na kushangazwa na utajiri mkubwa wa uoto wa asili kwenye udongo mwekundu uliojaa neema ya rutaba. Pamoja na uwepo wa wakimbizi kwenye eneo kubwa la wilaya ya Kibondo, wakazi wa wilaya hiyo hawajaathirika sana na upungufu mkubwa wa chakula katika maeneo yao. Hii inatokana na hali nzuri ya hewa na kutumia aina bora ya zao la muhogo kutoka Nigeria lenye kuhimili ukame na kutoshambuiiwa na wadudu.

Mwaka 2005, kikundi cha *'Kibondo Big Power Group'* kilianzishwa chini ya uongozi wa Mkuu wa Wilaya, Luteni Kanali mstaafu John Mzurikwao. Kikundi hiki chenye jumla ya vijana 25 waliokuwa wakifanya kazi mbalimbali kama wapiga debe, wazururaji, wacheza korokoro na wabeba mizigo kwenye kituo cha mabasi cha mjini Kibondo. Wazo la kuunda kikundi hiki lilitokana na mkuu huyo kuona hali tete iliyopo Kibondo mjini ambacho ni kitovu cha wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi na pia kuona ugumu wa kutofautisha wakimbizi wa kweli, wananchi na watu wasiowaaminifu. Hivyo aliamua kuhamasisha vijana ili kuunda kikundi cha vijana wenye ari ya kubadilisha hali zao za maisha kwa kuanzisha shughuli mbadala za kiuchumi.

Wakiongozwa na kijana shupavu aitwae Kennedy Sarundari, vijana walikutana na kujadiliana namna wanavyoweza kuanzisha shughuli mbadala ili kubadilisha mwelekeo wa maisha yao. Mkutano wa

>>> inaendelea uk. 11

## Juhudi za Kuondoa Umaskini kwa wakazi wa Jiji la Dar...

>>> inatoka uk. 8

sheria za halmashauri. NEMC ilitoa mwongozo wa namna ya kukagua mazingira na kutoa notisi kwa wakazi kadhaa wa jiji katika maeneo ya soko la Tandale na Kigogo na inafuatilia kuhakikisha zinafuatwa. Hii ilisaidia maafisa mazingira wa jiji kujua namna ya kutumia vifungu vya sheria ya mazingira namba 191 kudhibiti wachafuzi.

Ikumbukwe kuwa maeneo kama Buguruni karibu na mabwawa ya maji taka imekuwa na historia ya muda mrefu ya kuwa na milipuko ya kipindupindu ugonjwa ambao hugharimu wananchi wa maeneo haya pamoja na serikali kutumia gharama kubwa kwa matibabu. Magonjwa ya kipindu pindu na malaria yanazuilika kwa kuzingatia kanuni za afya na kuondoa mazalia ya mbu na kuweka mazingira.

Aidha kuweka miundo mbinu ya maji safi na salama kutasaidia kupunguza uchimbaji holela wa visima vifupi na matumizi ya maji ya visima ambayo mara nyingi si salama kwa afya.



*Uchafu uliotupwa karibu na Soko la Tandale ni tishio kwa afya na Mazingira (picha kutoka maktaba ya NEMC).*

## Kupunguza Gesijoto Kupitia Kudhibiti Ukataji Miti...

>>> inatoka uk. 7

juhudi za jumuiya ya kimataifa katika kupunguza uzalishaji wa gesijoto; kusaidia juhudi za nchi katika kusimamia misitu; na kuchangia katika juhudi za nchi katika kupunguza umasikini na kukuza uchumi.

Tanzania inatekeleza programu mbili za kupunguza gesijoto kupitia udhibiti wa ukataji miti ovoy na uharibifu wa misitu. Programu hizo ni ile ya ushirikiano wa Tanzania na Norway na ile iliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UN-REDD). kupitia programu ya ushirikiano wa Tanzania na Norway, Tanzania itapokea jumla ya dola za Marekani milioni 100 kwa kipindi cha miaka mitano ili kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na inayohusu kujenga uwezo, kuhamisha tekinolojia ili kusaidia kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa taarifa pamoja na kufuatilia utekelezaji, kuandaa na kutekeleza programu ya miradi ya majaribio pamoja na namna ya kuwasaidia wananchi kifedha ili waweze kutekeleza shughuli mbalimbali chini ya mfumo huu. Programu ya UN-REDD itasaidia kukamilisha baadhi ya shughuli kwa mfano masuala ya utafiti na mengineyo.

Ili kuratibu vema utekelezaji wa shughuli chini ya mfumo huu, Serikali iko katika mchakato wa kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa REDD. hadi sasa, hatua zifuatazo zimechukuliwa: kuanzisha Kikosi kazi cha Kitaifa ili kusiamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za REDD katika kipindi cha majaribio nchini; kuandaa mwongozo wa kitaifa wa REDD ambao pamoja na mambo mengine, unabainisha shughuli ambazo zinaweza kutekelezwa katika kipindi cha majaribio, vigezo vya taasisi zinazoweza kushiriki katika kutekeleza miradi ya majaribio, mada zinazoweza kufanyiwa kazi, pamoja na maeneo au misitu ambako shughuli hizo zinaweza kufanyika. Aidha, unabainisha masuala mengine kama uratibu, upatikanaji wa soko, ulipaji wa fedha, kujenga uwezo, kufuatilia utekelezaji na kutoa taarifa. Shughuli nyingine ambazo zimetekelezwa ni kutoa matangazo ili kukaribisha maombi ya miradi kutoka kwenmye Asasi Zisizo za Kiserikali (AZAKI) na taasisi nyingine. Hadi sasa, miradi 11 iko katika hatua za mwisho za kupewa fedha na hivi karibuni zitaanza kutekelezwa.

Kupitia mpango huu wa REDD, mchakato wa kutengeneza tovuti unakamilishwa. Tovuti hii itatoa nafasi kwa taasisi zinazotekeleza shughuli za REDD kubadilishana taarifa na uzoefu, pamoja na mafanikio na changamoto zilizopo. Zaidi ya hayo, tovuti hii itakuwa ni njia ya wadau kujielimisha kuhusiana na REDD na namna ambayo wanaweza kushiriki katika kutekeleza shughuli mbalimbali za aina hiyo. Aidha, Kikosi kazi kimeandaa utaratibu wa kutembelea maeneo mbalimbali nchini na kushiriki karika shughuli mbalimbali za kukuza weledi kupitia vyombo vya habari na njia nyingine ili wadau waweze kushiriki katika utekelezaji wa REDD nchini.

Siku za usoni, AZAKI, vyama vya kiraia, serikali za mitaa, vijiji na taasisi za kiserikali, makampuni binafsi, na wananchi kwa ujumla watafaidika kupitia mfumo wa REDD watakapotekeleza shughuli mbalimbali zinazolenga kuimarisha utunzaji wa misitu kwa kupunguza ukataji miti na uharibifu wa misitu. Hapo baadaye, shughuli nyingine zinazohusiana na upandaji miti, uhifadhi wa misitu na usimamizi endelevu wa misitu zitakuwa sehemu ya utekelezaji wa REDD. Faida katika utaratibu wa REDD itapatikana kupitia mfumo wa kupima kiasi cha hewa mkaa kilichopunguzwa baada ya kutekeleza shughuli zinazolenga upunguzaji. Mfumo wa kufuatilia, kutoa taarifa na kuthibitisha kuhusu utawekwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidika kutokana na juhudi zao za utunzaji na usimamizi endelevu wa misitu.

Utaratibu wa kupunguza gesijoto kupitia kudhibiti ukataji miti na uharibifu wa misitu uliokubaliwa na jumuiya ya kimataifa, ni mpya na unalenga kukabili tatizo la mabadiliko ya tabianchi kwa kutoa vivutio kwa nchi zinazoendelea zinazotunza misitu. Utaratibu huu unatarajiwa kuwa sehemu ya mpango wa kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi baada ya mwaka 2012 unaotarajiwa kupitishwa katika Mkutano wa 15 wa nchi zilizoridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi mjini Copenhagen Desemba mwaka huu. Kupitia utaratibu huu, Tanzania kwa ujumla, na wananchi katika maeneo yao, wanatarajiwa kufaidika kupitia utekelezaji wa vivutio vitakavyokuwa vinatolewa kutokana na usimamizi endelevu wa misitu. Wananchi, AZAKI, vyama vya kiraia na wadau wote wanashauriwa kutumia fursa hii ili kufaidika pamoja na kusaidia maendeleo ya nchi kwa ujumla.

# Utunzaji wa Mazingira Wasaidia Vijana Kujitegemea...

>>> inatoka uk. 9

awali uliwahusisha vijana takriban 100, ambapo baada ya kubalishana mawazo walikubaliana kuanzisha kilimo cha ushirika, ambapo wangepata maendeleo katika kilimo cha pamoja kama njia mbadala ya kujikimu. Baada ya kukubaliana waliwasilisha maombi yao Wilayani na kupewa ardhi kiasi cha ekari 200 kwenye eneo lililopo kilomita 26 nje ya mji wa Kibondo. Uongozi wa wilaya uliwawezesha wanakikundi kukamilisha taratibu zote za kisheria ili kuhakikisha umiliki wa eneo lao na pia kuwapatia vitendea kazi (majembe na mapanga) vya kuanzisha shughuli. Kazi ya kubomoa msitu ilikuwa nzito sana kiasi cha kuwasambaratisha vijana wengi na hatimaye kubakia na vijana 25 tu. Ili kupata mwongozo katika uanzishaji wa shughuli hii, Wilaya iliwapatia Afisa ugavi wa kilimo



*Uvunaji wa mihogo*

ambaye amekuwa akifanya nao kazi katika hatua zote za shughuli za uendelezaji wa eneo hilo. Pamoja na maelekezo, vijana hawa walisaidiwa kupata aina sita za miche ya mihogo ambazo zimepandwa katika maeneo tofauti ili kupima uwezo wa uzalishaji, uwingi wa mavuno na uhimili wa maradhi mbalmbali.

Baada ya mwezi mmoja Mkuu wa Wilaya, ambaye pia ni mlezi wa kikundi hicho, alifurahishwa kukuta vijana wamelima eneo la ekari 26. Ili kufanikisha kazi hii, vijana wamejiwekea mkakati wa kufanya kazi kwa kuhakikisha kwamba:

a) Wote wanashiriki kulima kwa siku maalumu kwa wiki na kugawana kazi kwa eneo la kulima kwa usawa.
b) Wanaruhusiwa kutoa pesa badala ya wao kufanya kazi katika eneo fulani kufuatana na makubaliano
c) Usimamizi wa shughuli za utendaji kufanyika kwa zamu
d) Mikutano ya majumuisho na taarifa mbalimbali hutolewa mara moja kila mwezi na kuwasilishwa mbele ya wanachama wote
e) Uongozi wa kikundi hufanyika kwa zamu kufuatana na uwezo wa mwanachama.

Ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa kazi kikundi kilijenga vibanda vya muda na banda la kulindia shamba.

Mnamo mwaka 2006 mwaka mmoja baada ya kuanzishwa kwa shughuli, kikundi, kilibahatika kutembelewa na Rais J. Kikwete akiwa ziarani mkoani Kigoma. Rais alifurahishwa na juhudi za kikundi, aliwaunga mkono kwa kutoa Shs. millioni mbili ili kuwasaidia kujiendeleza katika kazi za upanuzi wa shughuli za shamba. Kwa wakati huo, shamba la Big Power Group lilikuwa limefikia ekari 96 Naye Mkuu wa Mkoa alitoa baiskeli 6 kuwasadia .

Wakati wa nilipowatembelea vijana hawa, 2007 shamba lao lilikuwa na ukubwa wa ekari 126. Ili kutenganisha aina mbalimbali za mhogo, kikundi kiliacha eneo huru lenye upana wa kutosha ambapo ilipandwa miti ya matunda na mbao na kuachia nafasi ya kutosha kwa kila aina ya mhogo. Hivyo aina mbalimbali za mhogo zimepandwa katika maeneo tofauti, ili kuzuia uambukizo wa magonjwa ya mimea.

Walipoulizwa motisha ya kufanya shughuli hizo ngumu kwa kutumia vitendea kazi duni, wana-kikundi walielezea kuchoshwa na majina yasiyopendeza kama vile:vibaka. Walisema kwamba kwa kufanya kazi wanajenga *'wasifu wao upya'* kwani kazi waliyoanzisha ni muhimili mkubwa wa nchi yetu. Waliendelea kuelezea kwamba kazi wanazofanya sasa zitawasaidia kuboresha maisha wao wenyewe, na wasipofanikiwa wao kama kikundi, watawarithisha watoto wao kazi ambayo watajivunia.. Waliendelea kueleza kwamba wangependa watoto wao wajivunie ukweli kwamba wazazi wao walianzisha mabadiliko ambayo yamebadilisha muelekeo mpya wa maisha. Waliamini kwamba endapo watafanikiwa katika kazi

>>> inaendelea uk. 13

# Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Hifadhi ya Mazingira katika Uchimbaji Madini kuchangia Juhudi za uchimbaji endelevu Tanzania

**Na Ladislaus Kyaruzi**



*Uharibifu wa mazingira kutokana na uchimbaji halamu wa madini katika msitu wa hifadhi wa Matabe, Biharamulo, mkoa wa Kagera-Disemba 2006*

Sekta ya madini hasa uchimbaji mkubwa hapa Tanzania ni sekta inayokua kwa kasi na inayochangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi. Mwaka 2005/2006, sekta ya madini ilichangia karibia asilimia 3.5 ya pato la taifa na ilifikia asilimia 42.4 ya bidhaa zilizosafirishwa nje ya nchi kwa mwaka huo. Dira ya sekta ya madini kuelekea 2025 inalenga kuchangia asilimia 10 ya pato la taifa. Ukuaji wa sekta hii kwa kipindi cha miaka ijayo unalenga katika kutosheleza mahitaji ya nishati; kwa kuanzisha uchimbaji wa makaa ya mawe, gesi na kuongeza utafiti wa mafuta. Zaidi ya muongo mmoja uliopita, mahitaji ya madini yameongezeka kwa kasi ya ajabu ambayo matokeo yake yanaifikia Tanzania. Kama zilivyo nchi nyingine zinazoendelea, Tanzania imeweka mifumo inayofungua milango ya biashara na uwekezaji kutoka nje ya nchi. Ili kunufaika na mwelekeo mpya wa kuendeleza uchimbaji madini Afrika, sekta ya madini nchini imeamua kuweka njia ya kuvutia wawekezaji ikizingatia mabadiliko ya uchimbaji wa madini wa kisasa.

Uzoefu unaonyesha kwamba, shughuli za uchimbaji madini husababisha uharibifu wa mazingira. Baadhi ya athari zitokanazo na uchimbaji wa madini ni uharibifu wa ardhi, uchafuzi wa maji na hewa, upoteaji wa bioanuai, uharibifu wa mandhari na miundombinu pamoja na kuingilia shughuli za kijamii na kiuchumi katika eneo husika. Uchimbaji wa madini endelevu ni

>>> inaendelea uk. 13

muhimu ili kulinda mazingira na kuleta maendeleo endelevu. Hivyo basi, ni muhimu kutambua na kutumia njia bora za utunzaji mazingira katika uchimbaji madini Tanzania.

Serikali imechukua juhudi mbalimbali za kufikia uchimbaji endelevu. Mwaka 1997 Serikali ilitunga Sera ya Mazingira ya Taifa mwaka 1997. Sera hii inasisitiza umuhimu wa kuhuisha masuala ya mazingira katika sera nyingine na programu mbalimbali ili kufikia uchimbaji madini ulio endelevu na shirikishi. Sera ya Mazingira inajumuisha majukumu ya kisekta kama sekta ya madini katika kuhakikisha masuala ya mazingira yanaaangaliwa na kutekelezwa. Sera inabainisha kuanzishwa kwa Sheria ya Mazingira ambayo inaainisha majukumu ya taasisi na wadau wengine katika kutunza mazingira.

Sheria ya Mazingira (Sura 191) ya mwaka 2004 imeweka majukumu ya kisheria ya kutunza mazingira katika shughuli za uchimbaji madini. Pamoja na mambo mengine Sheria inasisitiza kuwa mtu yeyote au mwekezaji wa mradi wowote ikiwa ni pamoja na uchimbaji madini anapaswa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kwa mujibu wa sheria kwa gharama zake mwenyewe kabla ya mradi kuanza kutekelezwa. Aidha, sheria inaitaka miradi yote iliyoanzishwa kabla ya sheria hii kufanya ukaguzi wa awali. Sheria ya Mazingira inatekelezwa kwa mujibu wa katiba ya nchi na inatekelezwa pamoja na sheria zingine za kisekta zinazolenga kutunza mazingira. Kibali au leseni ya

>>> inaendelea uk. 14

## Utunzaji wa Mazingira Wasaidia Vijana Kujitegemea...

>>> inatoka uk. 11

waliyoianzisha kitazaliwa kijiji cha biashara chenye misingi bora ya uzalishaji.

Vijana walikiri kwamba wanatambua umuhimu wa kuwa na nidhamu ya hali ya juu na wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii . Walipoulizwa endapo wana katiba inayowaongoza katika kuendesha shughuli walijibu kwamba ingawa wanaelewa umuhimu wa katiba lakini wanatambua kwamba kinachotakiwa ni makubaliano na imani ya kikundi katika kuamini wanachokifanya. Pia walieleza kuwa lengo ni kubadilisha msimamo wa kubadili muelekeo wa maisha yao ingawa maandiko huongeza tu msisitizo kwa wahusika katika swala wanalolenga kufanikisha. Wao wanaamini katika falsafa ya utaratibu waliojiwekea unaozingatia kwamba :

1. Hakuna sukari bila kutoa jasho;
2. Kujenga msingi kwa ajili ya watoto wao
3. Asiyechangia asifaidike na jasho la mtu mwingine

Bango lililowekwa mwanzoni mwa shamba lao linaonyesha picha kubwa ya kalamu yenye ncha kali na mwisho wa kalamu kuna alama ya jembe. Maelezo yao ni kwamba kukosa elimu kusiwe sababu ya kushindwa kufanya shughuli za kujiendeleza na kwamba kwa mtu aliyekosa elimu ya darasani anayo nafasi, uwezo na motisha wa kujishughulisha na kujiendeleza kwa njia mbadala za uzalishaji.

Nia ni kutafuta uwezekano wa kusaidiwa kuanzisha ujenzi wa nyumba ndogo ndogo kwa ajili ya familia chache za watakaosimamia shughuli, ujenzi wa ghala kwa ajili ya vifaa na kuhifadhi mazao yanapovunwa, sehemu za kukaushia mihogo na kuhifadhi kabla ya mauzo. Kikundi pia kinaangalia uwezekano wa kusaidiwa kupata mitambo ya kusaga na kusindika mhogo kwa ajili ya mauzo pale pale mjini na kuuza kwenye soko la nje.

**Shuguhuli za uhifadhi**

Ni kweli usiopingika kwamba mali asili ni mhimili mkubwa wa maisha ya mwanadamu, pamoja na kutoa muelekeo kwa wananchi wengi waishio vijijini. Kundi hili la vijana walikubaliana kutenga eneo kubwa la msitu wao kwa ajili ya uhifadhi, ufugaji wa wanyama na uzalishaji wa asali. Kwa ajili hiyo tahadhari ilichukuliwa wakati wa kufyeka msitu kuhakikisha kwamba miti yote ya asili yenye matunda na madawa asilia haikukatwa. Pia Kikundi cha Big Power Group kina mipango madhubuti ya kutumia msitu uliohifadhiwa kwa kulishia mifugo.

Ingawa haikutarajiwa, eneo walilogawiwa linapakana na msitu wa hifadhi ya (Moyowosi), Nature reserve, Big Power Group wamejipa kazi ya ulinzi wa eneo hili wakiunda eneo linalotenganishwa hifadhi na vijiji vya jirani na mji wa Kibondo ili kuhifadhi bionuai ya eneo hilo. Hivyo wamejipa kazi ya kulinda eneo hili kutokana na majangili, wawindaji na wavamizi wengine.

## Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Hifadhi ya Mazingira...

>>> inatoka uk. 13

kufanya mradi au shughuli yoyote kwa mujibu wa sheria yoyote haitampa mwekezaji au mwenye mradi haki ya kuanza kutekeleza mradi au shughuli bila Hati ya Tathmnini ya Athari kwa Mazingira iliyotolewa na Waziri mwenye dhamana ya mazingira nchini. Tathmini ya Athari kwa Mazingira inafanywa na mtaalam wa mazingira aliyesajiliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mwaka 2001, serikali iliongeza juhudi zaidi kwa kuanzisha Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Hifadhi ya Mazingira katika uchimbaji madini. Lengo la Tuzo hii ni kutambua juhudi za kampuni au mtu binafsi aliyefanya vizuri zaidi katika uboreshaji wa hifadhi ya mazingira, na mafanikio yake katika uendeshaji endelevu wa shughuli za uchimbaji madini. Aidha, Tuzo ina lengo la kuhamasisha makampuni na watu binafsi kutambua na kuona umuhimu wa kuendeleza uchimbaji madini ulio endelevu. Kupitia Tuzo hii, serikali inatafuta jinsi ya kusaidia wachimbaji na kutoa motisha kwa wachimba madini kujumuisha masuala ya mazingira katika shughuli zao za uchimbaji madini.

Kamati ya Uteuzi yenye wajumbe watano iliyoundwa na Rais hufanya kazi ya kumtambua mshindi wa Tuzo kila mwaka. Kamati hii inasaidiwa na Kamati ya wataalam kutoka taasisi mbalimbali za serikali, vyuo vya elimu ya juu na taasisi binafsi.

Katika kutoa Tuzo na Vyeti kwa washindi inayotolewa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kuna makundi matatu mbayo ni makampuni makubwa, ya kati na wachimbaji wadogo wadogo yanayotambuliwa kulingana na leseni ya uchimbaji. Aidha, kuna madaraja manne ya zawadi ambayo ni Tuzo ya Rais, Cheti cha Ustahili, Cheti cha Kutia moyo (kwa mshindi wa wachimbaji wadogo wadogo) na Cheti cha Ushiriki.

Makampuni yote yanayofanya shughuli za uchimbaji madini nchini yanapaswa kushiriki. Yanahitajika kuandaa taarifa fupi kulingana na vigezo na miongozo ya Tuzo na kuikabidhi kwa kamati ya wataalam inapotembelea sehemu zao. Makampuni makubwa na ya kati kila moja hutoa Dola za kimarekani 2,000 kila shindano kama mchango wa kushiriki. Baadhi ya fedha hizi hutumika kumzawadia fedha taslimu mshindi wa wachimbaji wadogo anayepata jumla ya alama zisizo pungua asilimia 70 ya alama zote.



*Uchimbaji wa madini uliozingatia taratibu za utunzaji na uhifadhi wa mazingira*